JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. MM/MC/PF/L1/8/105** Tarehe: 25/11/2021

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anawatangazia waombaji wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani kuleta maombi ya kazi kwa nafasi zilizoainishwa hapo chini, baada ya kupata kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/362/01"B"/14 cha tarehe 15 Octoba , 2021 , kutoka kwa Katibu Mkuu UTUMISHI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu ajira mpya. Hivyo basi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi husika kwa nafasi zifuatazo:-.

### MTENDAJI WA MTAA DARAJA LA III (NAFASI 1)

i. **Sifa za kitaaluma za mwombaji.**

a) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
b) Awe amepata mafunzo ya stadi ya kazi ngazi ya Cheti katika fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Rasilimali watu, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali.

ii. **Mshahara.**
Ngazi ya mshahara TGS B1 (Mshahara kwa mwezi Tsh. 390,000/=)

iii. **Majukumu ya Mtendaji wa Mtaa Daraja III**
a) Atasimamia utekelezaji wa Sera za Halmashauri
b) Ataishauri Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo ya Mtaa
c) Atasimamia utekelezaji wa sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika eneo la Mtaa
d) Ataishauri Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya ulinzi na usalama
e) Atasimamia utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umaskini
f) Atakuwa Afisa Mhasibu wa Kamati ya Mtaa
g) Ataandaa na kutunza Rejesta ya wakazi wote wa Mtaa
h) Atakuwa msimamizi wa wataalam wanaofanya kazi
i) Atasimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.

Kiwanja Na 168 na 171 Kitalu "K" Chikongola, Makutano ya Barabara ya Tanu na Chikongola S L P 92, Mtwara. Simu: +255 232333102, Nukushi +255 23 2334794
Baruapepe: md@mtwaramikindanimc.go.tz Tovuti: www.mtwaramikindanimc.go.tz

Scanned with CamScanner

j) Atakuwa Mtendaji Mkuu katika Mtaa.
k) Atafanya kazi yoyote atakayoagizwa na Katibu Tarafa au Mkurugenzi wa Halmashauri

## KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III NAFASI (1)

i. **Sifa za kitaaluma za mwombaji.**

a) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
b) Awe amepata mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya tatu. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kishwahili na Kingereza maneno 89 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Komputa kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika Program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

ii. **Mshahara.**

Ngazi ya mshahara TGS B1 (Mshahara kwa mwezi Tsh. 390,000/=)

iii. **MAJUKUMU YA KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III**

a) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
b) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
c) Kusaidia kutunza kumbukumbu / taarifa za matukio , miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
d) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada , nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
e) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya , kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
f) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi

## MTEKNOLOJIA MAABARA DARAJA LA II – (MKATABA ) - (NAFASI 1)

i. **Sifa za mwombaji**

Awe amehitimu Stashahada (Diploma) ya Uteknolojia katika fani ya Maabara kwa muda usiopungua miaka 2 kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambaye amesajiliwa na baraza husika la kitaaluma.

ii. Posho kwa mwezi Tshs 400,000/=

iii. **KAZI NA MAJUKUMU**

(i) Kupima sampuli zinazoletwa maabara.

(ii) Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu.

(iii) Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali



Scanned with CamScanner

(iv) Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.

(v) Kufundisha watumishi walio chini yake.

(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

## MTEKNOLOJIA MSAIDIZI- MAABARA (NAFASI 1) – (MKATABA)

i. **Sifa za mwombaji**

Kuajiriwa wenye cheti katika fani ya Maabara kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza yao pale inapohusika.

ii. Posho kwa mwezi Tshs 300,000/=

iii. **KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kuaandaa vitendanishi (reagents) vya kufanyia vipimo vya MAABARA
2. Kufanya kazi za awali sampli zinazotolewa maabara
3. Kukusanya damu kutoka kwa wagonjwa na watu wanaojitolea
4. Kurekodi matokeo ya vipimo kwenye regista
5. Kutayarisha vifaa vya kazi
6. Kuhifadhi kwa mujibu wa taratibu sampuli zote zinazohitaji kuhifadhiwa baada ya uchunguzi
7. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

## MASHARTI YA JUMLA YA MUOMBAJI WA NAFASI ZA KAZI

a) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na wasizidi umri wa miaka 45.
b) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi mahali popote pale ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani
c) Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, Kidato cha Nne na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyohusika.
d) Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.



Scanned with CamScanner

e) Waombaji waambatanishe na picha ndogo 2 passport size zilizopigwa hivi karibuni.

*f)* ***"Testimonials" " provisional results", "statement of result"*** Hati ya matokeo ya kidato cha Nne **"result slip" Havitambuliki.**

g) Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa

h) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha Taaluma ambao vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) NA Baraza la Elimu ya Ufundi(NACTE)

i) Waombaji waliofukuzwa kazi, kupunguzwa au kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi.

j) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa tu kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi

k) Watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usahili

l) Uwasilishaji wa taarifa za kughushi utaadhibiwa kisheria , aidha , maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kingereza na yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja Masijala ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara- Mikindani au kutumwa kupitia posta kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P 92,
**MTWARA-MIKINDANI**

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 10/12/2021 saa 9:30 Alasiri**

COL Emanuel H. Mwaigobeko
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**MTWARA-MIKINDANI**



Scanned with CamScanner